# *MWONGOZO WA KUTENGENEZA HEI*

Nyasi nzuri za kutengeneza hei ni kama zile za Rodesi, Sainodoni na Brakiaria. Nyasi hizi hukauka haraka bila kupoteza thamani yake kwa kiwango kikubwa ili kutengeneza na kuhifadhi hei nzuri mfugaji anashauriwa kufuata hatua zifuatazo:

1. Kata nyasi mara tu zinapoanza kuchanua ili kupata hei nyingi kwa eneo na yenye viini lishe vingi.
2. Kausha nyasi juani huku ukigeuza kila siku mara moja hadi mbili. Lengo ni kupunguza maji kwenye nyasi hadi chini ya asilimia 15. Nyasi fupi zinaweza kukauka vizuri kwa siku tatu hadi nne na nyasi ndefu zinaweza kuchukuwa siku tano hadi sita kutegemeana na hali ya hewa.
3. Tengeneza hei wakati wa kuanza msimu wa kiangazi ili kukwepa mvua wakati wa kukausha nyasi. Nyasi zilizokauka zikinyeshewa na mvua huota ukungu hay kuharibika.
4. Hakikisha hei imekauka vizuri. Tambua hei iliyokauka vizuri kwa kukwaruza mashina ya nyasi kwa kutumia kisu kidogo. Kama ganda la shina halitoki kirahisi basi nyasi zitakuwa zimekauka vizuri na kua hei.
5. Baada ya kukauka funga mizigo maalumu ya hei (yaani beili) kwa beila au boksi maalumu la mbao. Ujazo wa boksi ni sm 75 x sm 45 x sm 35-39.
6. Hifadhi beili katika banda zuri ambalo linapitisha hewa vizuri na halivuji. Weka beili juu ya kichanja ili kuruhusu hewa kupita chini ya beili na kuendelea kuzuia unyevunyevu unaoweza kutokea hasa katika maeneo ya milimani ambapo baridi inaweza kusababisha ukungu.
7. Hakikisha banda la hei halipo karibu na jiko maana moto ni hatari kwa hei. Hei inachukua moto kwa haraka sana. Hivyo usivute au kupitisha moto karibu na banda la hei. Hakikisha banda hilo limefungwa vizuri baada ya kuchukua hei ya kulisha.

**Faida ya kufunga nyasi kavu katika beili**

1. Humwezesha mfungaji kuhifadhi malisho mengi katika nafasi ndogo

2. Humwezesha mfugaji kukadiria vizuri kiasi cha malisho yanayohitajika kwa msimu wote wa kiangazi. Kwa mfano kama ng'ombe mmoja wa maziwa anaweza kula kilo 8 za hei kwa kiangazi cha siku 180 (yaani miezi sita) atahitaji hei kila beili ikiwa na kilo 10.

3. Hupunguza gharama za usafirishaji wa malisho makavu toka mashambani

4. Humwezesha mzalishaji/mfugaji kuweka malisho yote ndani ya banda hivyo kuepuka uharibifu kutokana na jua aumvua kama angelirundika malisho hayo nje ya banda bila kufungwa beili.

**Ukitaka kufahamu zaidi wasiliana na:**
Idara ya Sayansi na Uzalishaji wa Wanyama, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, S.L.P. 3004 – Morogoro. Simu 023-2604617, 075430690,0763364980